



# MAMILAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MWANZA (MWAUWASA)



## UFAHAMU MNYORORO WA UZALISHAJI MAJI

Kumekuwepo na dhana mbalimbali mionganini mwa wananchi na hususan wateja, kuhusiana na namna ambavyo maji ya bombani wanayotumia kutoka MWAUWASA yanavyochakatwa hadi hapo yanapowafikia. Hivyo ni muhimu kila mtumiaji akaelewa hatua mbalimbali maji haya yanapitia kabla hayajamfikia bombani

### UTANGULIZI

NDUGU MTEJA, LEO TUNAKUELETEA ELIMU KUHUSU 'MNYORORO WA UZALISHAJI MAJI.' KUPITIA MIMI KWA KIASI KIKUBWA UTAPATA ULEWEWA WA HATUA MBALIMBALI ZA KUHAKIKISHA MAJISAFI NA SALAMA YANAKUFKIA BOMBANI.

## MWAUWASA

ASANTE SANA, KWELI NILIKUWA NA SHAKU KUBWA YA KUJUA KUTOKA KWENU NI NAMNA GANI MAJI SAFI NA SALAMA YANANIFKIA

Maji kutoka Ziwa Victoria ambayo ndio chanzo kinachotumiwa na MWAUWASA kwa wakazi wa Mwanza, utakubaliana na sisi kuwa maji haya ya ziwani si safi na salama kwa matumizi, hivyo ili kuyaboresha na kuyafanya yawe safi na salama, hatua kadhaa zinahitajika kuchukuliwa na hapa ndipo tunasema uongezaji thamani wa maji.

### Mabomba kutoka ziwani kwenda kituo cha kwanza hadi kituo tiba

HILI BOMBA LINATO MAJI HAPO KWENYE CHANZO KUELEKEA KATIKA KITUO TIBA. UMBALI KUTOKA KWENYE CHANZO HADII KWENYE KITUO CHA TIBA NI TAKRIBANI KILOMITA MOJA NA KWENYE MUINUKO WA MITA 85 NA PALE KWENYE CHANZO KUNA MABOMBA MAKUBWA MAWILI YENYE KIPENYO CHA MILIMITA 1100 AMBAYO YAMEINGIA NDANI YA ZIWA, UMBALI WA MITA 120

2

### HATUA 1: UZALISHAJI (UCHOTAJI WA MAJI KUTOKA ZIWANI)

Maji yanatoka Ziwa Victoria hivyo yanahitaji hatua ya tiba, teknolojia pia inahitajika


TAZAMA KULE! LILE JENGO NDIGO PALIPO NA MITAMBO YA KUSUKUMA MAJI GHAFI PIA NDIGO TUNAPOCHOTE MAJI (CHANZO CHA MAJI CAPRIPOINT) PANA MIUNDOMBINU NA MITAMBO YA KUSUKUMA ILI KUYAPELEKA KWENYE KITUO TIBA.



1

Mitambo mikubwa inatumika kwa namna iliyobuniwa, inatumia kiwango kikubwa cha nishati

HII NI BAADHI YA MITAMBO ILYOPO KWENYE VITOO VIKUBWA VYA KUSUKUMA MAJI IKIWEMO VITOO VYA MABATINI, NYEZEZI NA KONA YA BWIRU. UENDESHAJI WA MITAMBO HII HUIGHARIMU MWAUWASA ZAIDI YA MILIONI 600 KWA MWEZI



3

### Lazima maji yatibiwe kwa madawa maalum ili yawe safi na salama kwa afya ya binadamu

HAYA NI MADAWA YA CALCIUM HYPOCHLORITE, DAWA HIZI HUTUMIKA KUYAFANYA MAJI KUWA MEUPE. NA KUNA MADAWA MENGINE YAPO KWENYE MIFUKO YANAITWA ALUMINIUM SULPHATE, HAYA NI KWA AJILI KUUA VIJIDUDU NA VIMELEA AMBAVYO VIPO KWENYE MAJI. MADAWA HAYA TUNAAZIZA KILA BAADA YA MIEZI MITATU TANI 25 AMBAZO HUGHARIMU MILIONI 144



5

### HATUA 2: KUTIBU

Kabla ya hatua zingine maji lazima yachujwe ili kuondosha taka kubwa, ikiwemo magugu maji na uchafu mwinge wenyewe kuleta madhara ya afya kwa binadamu.

TAZAMA KULE! YALE NI MACHUJIO YA MAJI. MAJI YAKITOKEA ZIWANI KABLA HAJATIBIWA NI LAZIMA YACHUJWE KWANZA, MACHUJIO YALE HUFANYA KAZI KWA UMEME

4



### HATUA 3: USAMBАЗАJИ

Maji yakithibitishwa kuwa ni safi na salama huanza kusambazwa. Maji yanapitia vituo vikuu ya kuyapa kasi yaani booster station (kuyasukuma) ambavyo bila kipitia vituo hivyo, hayawesi kusafiri umbali mrefu kutokana na hali halisi ya jirofia ya Jiji la Mwanza kutokana na kuwepo kwa miinuko na miamba.

JENGO HILI NI BOOSTER STATION YA MABATINI NI MOJA YA VITOO VYA KUSUKUMA MAJI

6

KWA HIYO SISI WAKAZI WA MILIMANI NDIO VITOO HIVI HUFANYA KAZI KUBWA KUTULETA MAJI KULE JUU

NDIO KWA SABABU HUHITAJIKA NGUVU KUBWA SANA

### Usambazaji kwenye manteki

HILI NI TENKI LA KITANGILI, LINAPOKEA MAJI KUTOKA KITUO CHA KONA YA BWIRU. AMBACHO PIA KINAPELEKA MAJI KWENYE MATENKI YA KAWEKAMO NA IBANDA. KITUO CHA NYEZEZI, KINAPELEKA MAJI KWENYE MATENKI YA NYEZEZI NA MAJENGO MAPYA HUKU KITUO CHA MABATINI KIKIPELEKA MAJI KWENYE MATENKI YA NYASHANA, MJIMWEMA, IGOMA NA BUJORA

7



ASANTE SANA LEO NIMEPATA ELIMU AMBAYO SIKUIJUA KWANI SASA NIMEELEWA KWAMBA MWAUWASA HUINGIA GHARAMA KUBWA KUTUSAMBАЗИА MAJI KUTOKA ZIWANI HADI BOMBANI. KWAMBA HUWEZI KUCHOTA TU MAJI ZIWANI NA YA KUYASAMBАЗА KAMA WANANCHI WENGI TUNAVYOFIKIRIA

KUCHOTA NA KUNYWA MAJI KUTOKA ZIWANI BILA KUTIBIWA NI HATARI KWA AFYA YA BINADAMU



Maji ni uhaji, tutunze na kulinda vyanzo vyetu ya maji sambamba na miundombinu inayotufikishia huduma hii adhimu